

# WATOTO WETU NA SALA

Mtunzi
Abdulmalik Al-qaasim
Mfasiri
Mbwana Ahmad Urari

شبكة الألوكة
www.alukah.net

# أولادنا و الصلاة

## باللغة السواحلية


تأليف

عبدالملك القاسم

ترجمة

امبوانا أحمد أوراري



Conveying Islamic Message Society

P.o.Box 834 - Alex - Egypt

E-Mail:info_en@islamic-message.net

E-Mail:cims_eg@yahoo.com

Site: www.islamic-message.net

Not for sale يُهدى ولا يُباع

www.alukah.net
شبكة الألوكة

# WATOTO WETU NA SALA

Mtunzi
Abdulmalik Al-qaasim
Mfasiri
Mbwana Ahmad Urari

# أولادنا و الصلاة

باللغة السواحلية

تأليف
عبدالملك القاسم
ترجمة
امبوانا أحمد أوراري



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net

شبكة الألوكة

بسم الله الرحمن الرحيم

Sifa njema anazistahiki Mwenyezi Mungu Mola wa viumbe vyote na rehema na amani zimfikie Mtukufu zaidi katika Mitume na Wajumbe, Mtume wetu Muhammad, Jamaa na Swahaba wake wote.

Watoto ndio pambo la maisha ya duniani, na wanapokuwa wema ndio hupatikana utulivu wa wazazi.

Ni jambo la kusikitisha kutokuwepo kwa watoto wa Kiislamu katika misikiti yetu. Kati ya watu wanaoswali, ni nadra kuwakuta wale ambao wako katika rika la barobaro! Nina'apa kwa Mwenyezi Mungu kuwa hii ni hali inayotoa tahadhari ya kuwepo kwa shari pana, uozo katika malezi na udhaifu wa umma wa Kiislamu



شبكة الألوكة - قسم الكتب

pale vijana hawa wasioswali watakapokuwa wakubwa. Wasiposwali leo wataswali lini pamoja na Jamaa ya Waislamu?

Kwakuwa dhambi kubwa na majukumu mazito yapo kwa wazazi, naikumbusha nafsi yangu na walezi wa familia kuhusu Hadithi ya Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa : " **Kila mmoja wenu ni mchungaji na ataulizwa juu ya anachokichunga. Na mwanaume ni mchungaji katika familia yake na ataulizwa juu ya anachokichumga**". Ameipokea Hadithi hii Bukhaariy na Muslim. Na Mwenyezi Mungu aliyetukuka anasema katika uteremsho mtukufu kwamba: "**Enyi ambao mmeamini, zikingeni nafsi zenu na familia zenu na moto (ambao) kuni zake**



شبكة الألوكة - قسم الكتب

**ni watu na mawe. Wasimamizi wa moto huo ni malaika wenye nguvu, wakali, hawamuasi Mwenyezi Mungu anapowaamrisha na wanatekeleza wanayoamrishwa** ". Qur'an, Sura At-tahriim (66),

Na katika mazungumzo ya wazi kutoka kwa Mtume wa umma huu (wa Kiislamu) anayoyaelekeza kwa kinababa na kinamama anasema: "**Waamrisheni watoto wenu kuswali na ilhali wao ni watoto wa miaka saba. Na wapigeni kwa ajili yake (kwa kukataa kuswali) na ilhali wao ni watoto wa miaka kumi**". Ameipokea Hadithi hii Imam Ahmad. Katika maelekezo haya matukufu ya Mtume, kuna mambo mengi mazuri ya jinsi ya kuwa mpole kwa mtoto na kwenda naye hatua kwa hatua**.** Mtoto analinganiwa kuswali akiwa na miaka

saba, na hapigwi kwa ajili ya swala isipokuwa tu anapofika miaka kumi katika umri wake. Katika kipindi hiki cha miaka mitatu, mtoto anakuwa amelinganiwa kwenye swala na imependezeshwa kwake zaidi ya mara elfu tano. Hivi mwenye kudumu kuswali katika miaka mitatu kwa namna endelevu na mfululizo, baada ya swala elfu tano, anahitaji kupigwa? Ni nadra kukuta katika wazazi anayeitekeleza Hadithi hii na akahitaji kumpiga mtoto baada ya miaka kumi. Hiyo ni kwa sababu mkusanyiko wa swala hizi ni mkubwa na kuzoea kwa mtoto mdogo kuswali na kwenda msikitini kutakuwa kupo katika damu yake, na ni sehemu ya ratiba ya maisha yake, na ni katika mambo yake makubwa zaidi.

Wengi leo wanampiga mtoto kwa sababu ya mambo madogo na ya kipuuzi

www.alukah.net
شبكة الألوكة

yasiyofikia daraja na umuhimu wa swala.

Anayeitafakari hali ya swala ya Alfajiri na wale watoto wa Kiislamu wanaoihudhuria swala hiyo, atausikitikia umma wa Kiislamu. Ni nadra kuwakuta katika misikiti vijana hawa ambao vijana kama wao walikuwa na uzito mwanzo wa umma (huu wa Kiislamu). Wako wapi akinababa na akinamama wanaowaamsha watoto wao na kulitilia mkazo suala hilo?

Imepokewa kutoka kwa (Swahaba) Ibn-abbaas, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: "**Nililala kwa mama yangu mdogo Maimuna. Akaja Mtume wa Mwenyezi Mungu, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, baada ya kuwa usiku umeingia na kusema: Je, kijana ameswali? Wakasema (kumjibu Mtume): Ndio**". Ameipokea Hadithi hii



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net
شبكة الألوكة

Abuudaauud. Na imepokewa kutoka kwa (Swahaba) Ibn-omar, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi yeye na mzazi wake, akisema kuwa: " **Mtoto anafundishwa kuswali anapojua kutofautisha kati ya kulia na kushoto kwake** ".

Wahenga Wema walikuwa wakiwafuatilia watoto wao katika swala na wakiwauliza. Imepokewa kutoka kwa Mujahid akisema kuwa: " **Nilimsikia mmoja kati ya Swahaba wa Mtume – akasema Mujahid; Nadhani si mwingine isipokuwa ni katika wale waliokuwepo katika vita vya Badri - akisema kumwambia mtoto wake kuwa: Je, umewahi kuswali pamoja nasi? Je, umeiwahi Takbira ya kwanza ? Akasema (mtoto): Hapana. Akasema (huyo Swahaba): Kheri ulizozikosa katika swala hiyo ni bora zaidi kuliko ngamia mia moja**



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net

**ambao wote wana macho meusi**".

Amesema Imam Adh-dhahaby katika kitabu chake Assiyar akinakili kutoka kwa Yaaqub naye akinakili kutoka kwa baba yake kwamba Abdulaziz bin Marwan alimpeleka mtoto wake Omar mjini Madina akasome huko. Alimwandikia barua Saleh bin Kisan awe akimfuatilia mtoto huyo. Alikuwa akimlazimisha kuswali. Siku moja mtoto akachelewa kuswali, akamuuliza: Ni jambo gani limekuzuwia (kuswali)? Akasema (yule mtoto): Mhudumu wangu alikuwa akichana nywele zangu. Akamwambia: Mfahamishe huyo anayechana nywele zako kuwa asifanye nywele zako kuwa ni bora kuliko swala. Na alimwandikia baba yake kumfahamisha hilo. Marwan alimtuma mjumbe na (mjumbe huyo) hakumsemesha yule mtoto mpaka



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net

alipozinyoa nywele zake.

Miongoni mwa mambo makubwa sana ambayo baba anaweza kumfanyia mwanawe ni kusuhubiana naye kwenda kuswali na kuwa naye jirani ili ajifunze kutoka kwake na amlinde asifanye mchezo na upuuzi.

Ewe baba na ewe mama, usikubali akatoka chini ya mikono yako kesho mtu asiyeswali. Mtapata dhambi kwa kumtoa kwa umma wa Kiislamu akiwa kafiri atokanaye na wazazi wawili Waislamu, kwa sababu tu ya uzembe na huruma ya uongo. Mnamuhofia asipatwe na baridi na kwa hiyo hamumuamshi kwa ajili ya swala ya Alfajiri! Mnamuhofia asipatwe na joto kali na kwa hiyo haendi kuswali swala ya Alasiri! "**Waambie: Moto wa Jahanamu ni mkali zaidi lau wangekuwa wanafahamu**". Sura At-tauba (9), aya 81.



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net
شبكة الألوكة

Imam Ibnulqayyim, Mwenyezi Mungu amrehemu, anasema kwamba: " **Anayepuuza kuwafundisha watoto wake mambo yenye manufaa kwao na akawaacha hovyo, basi ametnda uovu wa hali ya juu! Uharibifu wa watoto wengi unakuja kutokana na wazazi na kupuuza kwao na kutowafundisha faradhi za dini na sunna zake. Kwa hiyo, wamewapoteza wakiwa wadogo na hawakuweza kujisaidia wao wenyewe na hawakuweza kuwasaidia wazazi wao wakiwa wakubwa**".

Ewe baba na ewe mama, katika kuwahimiza watoto kuswali msikitini kuna faida kubwa. Miongoni mwa faida hizo ni hizi:

**1.** Kuzitakasa dhima (majukumu) zenu mbele ya Mwenyezi Mungu na kuepukana na dhambi baada ya kumfanya mtoto



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net
شبكة الألوكة

aipende swala na kumwamrisha kuswali. Amesema Imam Ibnutaimiyah, Mwenyezi Mungu amrehemu, kuwa: "**Na ambaye ana mtoto mdogo anayemmiliki au yatima au mtoto wa kuzaa halafu asimwamrishe kuswali, bila shaka mkubwa huyo ataadhibiwa kwa kutomwamrisha mtoto mdogo, na ata'aibishwa vikali, kwakuwa amemuasi Mwenyezi Mungu na Mtume wake**".

**2.** Kutaraji malipo ya kumzoesha kufanya ibada. Amesema Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: "**Mwenye kulingania (kuhubiri) uongofu atapata katika malipo mfano wa malipo ya watakaomfuata. Halitapunguza hilo katika malipo yao kitu chochote**". Ameipokea Hadithi hii Imam Muslim.

**3.** Kutambua kwamba mtoto yupo



شبكة الألوكة - قسم الكتب

katika ulinzi wa Mwenyezi Mungu na uchungaji wake siku nzima. Amesema Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: "**Yeyote anayeswali Alfajiri katika Jamaa, basi yeye yumo katika dhima (hifadhi) ya Mwenyezi Mungu**". Ameipokea Hadithi hii Imam Ibnumaajah.

**4.** Kumtoa mtoto katika kundi la makafiri na wanafiki atakapokuwa mkubwa, kama alivyosema Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa "**Ahadi iliyopo kati yetu(Waislamu) na kati yao(makafiri) ni swala. Kwa hiyo, mwenye kuiacha swala amekufuru (amekuwa kafiri)**". Ameipokea Hadithi hii Imam Ahmad. Na kama alivyosema Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa "**Hakuna swala iliyo nzito zaidi kwa**

**wanafiki kuliko (swala ya) Alfajiri na Ishaa. Na lau kama (watu) wangejua (ubora, umuhimu, mambo mema na mazito) yaliyomo katika swala hizo, basi wangeziendea japo kwa kusota**". Ameipokea Hadithi hii Imam Bukhaariy.

**5.** Kumlea mtoto katika kupenda kheri na mambo mema ili baada ya kufa kwenu awe kitegauchumi chenu. Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, ameweka sharti la **wema** kwa mtoto (ili aweze kumnufaisha mzazi wake), kama ilivyo katika Hadithi isemayo kuwa "**Wakati akifa mwanadamu, hukatika matendo yake isipokuwa katika mambo matatu**" na akataja katika mambo matatu hayo kuwa ni: "**au mtoto mwema atakayemuombea (mzazi wake)**". Ameipokea Hadithi hii Imam Muslim



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net
شبكة الألوكة

Miongoni mwa sababu zinazosaidia katika kumlea mtoto juu ya kuswali ni hizi:

**1.** Nyinyi wazazi muwe mfano mwema kwa watoto katika kuidumisha swala na kuipa umuhumu. Watoto wanapofika umri wa miaka saba na kuwa na fahamu, sheria inakutakeni muwaamrishe kuswali na kwenda nao misikitini, kwani mtoto anakua akiwa na yale aliyozoeshwa na baba yake.

**2.** Kuyapa umuhimu wa kwanza mambo ya akhera kuliko mambo ya kidunia katika kila jambo, na kuwalea watoto katika hilo na kulipandikiza katika nafsi zao. Isiwe mitihani ya shule ni muhimu zaidi kuliko swala, na isiwe kujisomea ni muhimu zaidi kuliko kwenda msikitini. Sio fahari mtoto wako kuwa kiongozi mkubwa na ilhali yeye ni miongoni mwa wanafiki wasiohudhuria



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net

swala (ya Jamaa) au makafiri wasioswali. Inakutosha kuwa ni fahari na ni heshima iwapo mtoto wako atakuwa anakula kutokana na chumo la mikono yake na huku akiwa anahudhuria Jamaa ya Waislamu (misikitini). Kama ataweza kukusanya yote mawili (kuwa kiongozi mkubwa na kuwa Mwislamu anayeswali Jamaa misikitini) ni vizuri zaidi.

**3.** Kuwa na uvumilivu. " **Na iamrishe familia yako kuswali na uwe na uvumilivu juu yake** ". Sura Taaha (9), aya 132. Amri ina uzito na usumbufu. Lakini pata habari njema, kwani Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema kuwa: "**Na wale ambao wanatoa juhudi kwa ajili yetu, tutawaonesha njia zetu**". Sura Al-ankabuut (29), aya 69.

**4.** Kuweka sababu zitakazosaidia kuamka. Miongoni mwa sababu hizo ni



شبكة الألوكة - قسم الكتب

kutokesha usiku, kuwa na saa ya kengele wakati wa Adhana au kabla ya Adhana na watoto kuwahi safu za mbele. Aliulizwa Sheikh Abdulaziz Bin-baaz swali lifuatalo: Baadhi ya watoto wanakwenda mapema (msikitini) siku ya Ijumaa na wanakuja watu wakubwa zaidi kuliko wao na kuwaondoa (kwenye safu) na kukaa wao kwenye nafasi zao wakitoa hoja ya kauli ya Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, isemayo kuwa: "**Wanifuate mimi (wawe nyuma yangu) katika nyinyi wale wenye balehe na utambuzi**" Muslim, Tirmidhiy, Abuudaauud. Je, jambo hili linafaa ? Akajibu kuwa: " **Wanayasema haya baadhi ya wanachuoni na wanaona kuwa ni bora zaidi kwa watoto kupanga safu nyuma ya watuwazima**. **Lakini kauli hii inahitaji kutazamwa upya. Jambo sahihi zaidi ni kwamba watoto wakiwahi safu**



شبكة الألوكة - قسم الكتب

za mbele, haifai kuwarudisha nyuma. Endapo watawahi safu ya kwanza au ya pili, haitakikani kwa wale wanaokuja baada yao kuwaondoa, kwa sababu wao wameiwahi haki ambayo hakuna aliyewatangulia. Hivyo, haifai kuwarudisha nyuma. Hayo ni kwa mujibu wa ujumla wa Hadithi (za Mtume s.a.w.) kuhusu suala hilo, na kwa sababu katika kuwarudisha nyuma kutapatikana kuichukia swala na kukosekana hali ya kushindana kwenda kwenye swala, na kwa hiyo jambo hilo halifai! Lakini kama watu watakuwa wamejumuika; kama vile wako safarini pamoja au wamejumuika kwa sababu yoyote, basi watajipanga safu watuwazima kwanza, halafu watoto, halafu wanawake baada yao, ikiwa itatokea hali hiyo na ilhali wamejumuika. Ama kuwatoa watoto katika safu na nafasi zao kushikwa na

**watuwazima ambao wamekuja baada yao, jambo hilo halifai kwa mujibu wa maelezo tuliyokwishaeleza. Ama kauli ya Mtume, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kwamba: " Wanifuate mimi (wawe nyuma yangu) katika nyinyi wale wenye balehe na utambuzi" muradi wake ni kuwahimiza watu balehe na wenye utambuzi (watuwazima) waharakishe kwenda kuswali na wawe watu wa mbele (wa mwanzo), na sio kwamba muradi wake ni kuwarudisha nyuma waliowatangulia kwa ajili ya wao kukaa mbele, kwa sababu kufanya hivyo kunapingana na hoja za kisheria tulizozitaja".**

**5.** Wafundishe watoto wako Hadithi zinazozungumzia swala na hukumu na adhabu ya mtu asiyeswali hapa duniani na Akhera. Wahamasishe wawe na matarajio



شبكة الألوكة - قسم الكتب

ya kupata malipo makubwa kwa mtu mwenye kudumisha swala. Wala usiseme kuwa wao ni wadogo, hawaelewi kitu. Wanaelewa, wanaweka kumbukumbu na wanahitaji kuhamasishwa ili kuzipa nguvu ari zao.

**6.** Wawekee zawadi na motisha ili waweze kudumu kuswali. Nakumbuka kwamba kuna mzazi mmoja alikuwa akiwapa watoto wake wadogo Riyali moja (sawa na shilingi 250/- za Kitanzania kwa sasa) kila siku kwa ajili ya swala ya Alfajiri. Matunda ya mapema ni kwamba mmoja wa watoto hawa amekuwa ni miongoni mwa maimamu wakubwa walio maarufu.

Nakumbuka pia kwamba kuna mama mmoja mjane alikuwa na mtoto mdogo yatima. Alikuwa akimpeleka kuswali swala ya Alfajiri kila siku. Mwenyezi Mungu alimkirimu mama huyu kwa sababu ya

www.alukah.net
شبكة الألوكة

mtoto huyu kwa kuweza kuhifadhi kitabu cha Mwenyezi Mungu na mtoto huyo hivi sasa ni mmoja wa maimamu wa msikiti na ni miongoni mwa wanaomtendea sana mambo mema mama yake. Amesema (Swahaba) Abdallah Bin-masoud, Mwenyezi Mungu amuwiye radhi, kuwa: "**Wapatilizeni watoto wenu katika swala na wazoesheni mambo ya kheri kwani (kufanya) kheri ni tabia (ambayo mtoto anatakiwa kuzoeshwa)**". Ameipokea Athar hii At-tabaraaniy.

**7.** Kuwaombea watoto dua za kheri kila wakati, na wakati mwingine wafanye wayasikie maombi yako unapowaombea wema, uongofu, kupata msaada wa Mwenyezi Mungu na kufanya yaliyo sahihi. Miongoni mwa dua za Mitume na watu wema ni hii: "**Ewe Mola wangu, nifanye mimi niwe msimamishaji swala**



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net
شبكة الألوكة

**na katika kizazi changu (pia). Ewe Mola wetu, na yakubali maombi yangu** ". Sura Ibrahim (14), aya 40.

**8.** Wafungamanishe na marafiki wema wanaohifadhi Qur'an na wanaoswali Jamaa. Wahamasishe watoto hao kwa kuwapa zawadi na motisha, kwani wao ni watoto wa Kiislamu.

**9.** Waombee dua njema wakati unapowaamsha na wasomee baadhi ya aya za Qur'an na Hadithi, kama: "**Ewe mwanangu mdogo, simamisha swala**". Sura Luqmaan (31), aya 17. Wasikilizishe malipo makubwa yaliyotamkwa na ulimi wa Mtume wao, Mwenyezi Mungu amfikishie rehema na amani, kuwa: "**Wape habari njema wanaotembea katika giza kwenda misikitini kuwa watapata nuru kamili siku ya Qiyama**". Ameipokea Hadithi hii Abudaud.



شبكة الألوكة - قسم الكتب

**10.** Mfanye mama yao aone kwako kwamba wewe unajali suala la wao kuamshwa na kuswali, kwani hilo litamsaidia kuendelea kuwajali na kuwahimiza. Zishukuru juhudi zake na mhamasishe na ilhali wao wanasikia.

**11.** Ewe baba, kama ambavyo unatafakari huduma za karibu na nyumba yako, wakati wa kununua nyumba, basi kabla ya hayo fikiria msikiti na ukaribu wake na nyumba yako. Kwa sababu katika hilo, utapata msaada wa kufanya ibada na jambo la kuswali litakuwa jepesi hasa kwa watoto wadogo pia utakuwa mwepesi uwezekano wa kuwafuatilia endapo masafa yatakuwa mafupi.

**12.** Tambua kwamba mtoto wako umpendaye anawezakuwa ni kuni za Jahanamu kama atakuwa haswali "**Enyi mlioamini, jiokoeni nyinyi na familia**



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net

**zenu zisiuingie moto ambao kuni zake ni watu na mawe**". Sura At-tahriim (66), aya 6.

**13.** Jenga ushirikiano kati yako na kati ya Imamu wa msikiti katika kuwahamasisha watoto wako kwa upande wake na kuwapa motisha kwa kuendelea kwao kuswlai, ikiwa ni pamoja na kuswali swala ya Alfajiri. Hakuna kizuizi kama Imamu atazungumza akiwahimiza wazazi kuwapeleka watoto wao kuswali, halafu akawashukuru wazazi wanaowapeleka watoto wao na kuwataja watoto hao kwa majina yao.

Ewe baba, anasema Mwenyezi Mungu Mtukufu kuwa: "**Na iamrishe familia yako kuswali na uwe na uvumilivu juu yake**". Sura Taaha (9), aya 132. Kuwa na furaha na matumaini, kwani wewe upo katika njia bora "**Na wale ambao wanatoa**



شبكة الألوكة - قسم الكتب

www.alukah.net
شبكة الألوكة

**juhudi kwa ajili yetu, tutawaonesha njia zetu**". Sura Al-ankabuut (29), aya 69.

Tunamuomba Mwenyezi Mungu awafanye wake zetu na watoto wetu wawe wema na wawe kifurahisho cha macho yetu. Tunamuomba amfikishie rehema na amani Mtume wetu Muhammad, Jamaa na Swahaba wake wote.



شبكة الألوكة - قسم الكتب

هذا الكتاب منشور في

شبكة الألوكة

www.alukah.net